NM Jarida la kifasihi

Toleo La XIV
Novemba - MMXXII

# NGURUMO ya MWANDISHI

Tunakutakieni Christmass njema

na Mwaka Mpya wenye baraka!



## Ana kwa Ana

### Julius Gabriel Mwita

## Nguvu ya kitabu, Siri ya ujasiri wake

## YALIYOMO

**TAHARIRI**— Heri ya Krismasi na Mwaka Mpya—Uk 02

**MWANDISHI WETU**— Ramadhani Makoleko— Uk 03

**NEW IN TOWN**— Mimi ni Binti—Uk 04

Yaliyojiri Chanzige— Uk 04

**PITIO LA VITABU**— Vuta N'kuvute— Uk 05

**MAKALA**— Vitabu Kila Mahali, Kusoma Siachi Ng'o!— Uk 06 na 07

**RIWAYA:** Usiwe Muuaji— uk 08 na 09

**HADITHI FUPI:** 40 za Muuaji— Uk 10

**ANA KWA ANA**: Julius Mwita:Nguvu ya Kitabu, Siri ya Ujasiri wake—Uk 11

**RIWAYA:** Mpigambio—Uk 12 na 13

**MATANGAZO:** SHUBAKA LA VITABU—Uk 14

**KITABU NILICHOSOMA:** The Power Of Discipline & From Mopping Floors—Uk 16

**MATANGAZO:** Uk 17

**NGURUMO YA MWANDISHI**

**MHARIRI: RICHARD MWAMBE**

**MSAIDIZI: REY STANLEY**

**WASILIANA NASI**

**0766 974 865 AU 0672 160 016**

**WhatsApp: +255 734 550 514**

## TAHARIRI: Heri ya Krismasi na Mwaka mpya kwenu nyote…

Asalaam,

Imekuwa desturi kila ufikapo mwezi wa Disemba, watu kujiandaa kwa sikukuu kubwa mbili; Krismasi na Mwaka Mpya. Watu hununua nguo nzuri, hujiandaa kwa vyakula aina aina ili mradi tu kumshukuru Mungu kwa mema yake aliyowajalia mwaka mzima.

Kwa kweli inavutia sana. Lakini ningependa tu kuwakumbusha wazazi kuwa licha ya haya yote tunayoandaa tukumbuke kuwa hapo Januari kuna suala zito la ada za watoto shuleni na wengine kodi za nyumba au za ofisi ambazo tunatumia.
Vipi. Tumejipanga na siku kuu hizo pia?

Jambo ambalo nimejifunza katika utu uzima wangu ni kwamba, Watanzania bado hatujui mipangilio ya matumizi ya vipato vyetu. Hii utupelekea kuingia kwenye mikopo na kadhalika.

Sikukuu ni jambo jema sana, kuwafanya watoto wafurahi hata na sisi watu wazima kugonga cheers na kuangusha mbuzi na mapochopocho kibao. Lakini basi tuangalie na kile ambacho tunacho mfukoni mwetu ili tuweze kupangilia kuhusu Januari.

Watoto wetu daima huuzunika, husononeka na hata huathirika kisaikolojia wanapopewa taarifa kuwa baba/mama zao hawajalipa ada hivyo wasihudhurie masomo. Muda huo hakumbuki kama ulimnunuria gauni au suruali nzuri kwa sikukuu.

Hebu tubadilike kidogo, tujaribu kuwafundisha watoto kuwa siyo lazima kila sikukuu wavae nguo mpya ila wasisitizie kuwa unataka kuwalipia ada, ili wasome kwa bidii na mengine yote yatakuja baadae.

Kwa wale wazazi ambao bado hawajaanza kusomesha tukumbuke kwamba hili jambo ni la wote na wewe utalifikia. Jifunze kutenga kiasi kwa ajili ya mwanao, mfungulie akaunti benki ili imsaidie wakati ukifika.
Wazazi si kweli kwamba elimu bora ipo kwenye shule za kisasa tu, lah! Hata zile shule zetu za serikali nazo zina elimu tena iliyo bora zaidi, hivyo basi jitazame na hali yako, mkono wako wafika wapi. Usijilazimishe kupeleka mtoto Santi nanihii wakati uwezo huna, utateseka, utakopa, utaishi kwa shida na msongo wa mawazo. Kama hauna uwezo mpeleke mtoto kwenye shule unayoweza ili ifikapo januari usiumie sana mpaka raha ya maisha ikupotee.
Niwatakie sikukuu njema ya Krisimasi na Heri ya Mwaka Mpya.

**Ric Richard Mwambe,**
**Iringa Tanzania**

## MWANDISHI WETU: Ramadhani Makoleko



**Jina langu ni Ramadhan Makoleko 'Makoleko Kalibonge II'. Japo nilizaliwa mkoani Lindi** katikati ya miaka ya 1980, lakini kwetu ni Mikindani, Mtwara. Elimu yangu ni Shahada ya Kiswahili niliyotunukiwa baada ya kuhitimu masomo katika Chuo Kikuu cha Dodoma.
Kama ilivyo asili ya jambo lolote ndani ya watu wote duniani, kwangu pia ni vivyo hivyo.

Nilianza safari hii kwa kuandika hadithi kwa mtindo wa michoro nikiwa Shule ya Msingi Mnaida kabla ya kuandika bila michoro nilipokuwa sekondari. Japo ni kipaji lakini msukumo wa kuandika ulitoka kwa marehemu kaka yangu ambaye kabla ya mauti yake, alikuwa mtu aliyependa kusoma sana riwaya na hadithi. Tabia hiyo aliniambukiza na hatimaye nikaona hata mimi nilikuwa na uwezo wa kuandika ingawa kwa wakati huo sikupata muda mzuri wa kufanya hivyo.

Kuanzia 2013, baada ya kuhitimu Chuo, ndipo nilipata muda mwingi wa kuandika. Niliandika makala, hadithi fupi na riwaya. Mpaka kufikia mwaka huu wa 2022, nimeandika miswada ya riwaya zaidi ya kumi na tano. Lakini kazi zilizochapishwa ni mbili tu. Kazi yangu ya kwanza ya riwaya ilitoka mwaka 2018. Riwaya hiyo inayoitwa Pigo la Nafsi inahusu nguvu ya mapenzi katika kudhuru na kuponya. Imechapishwa na Oxford University Press, Nairobi, Kenya. Inapatikana kwa wingi huko.

Riwaya yangu ya pili ni Haki ya Dhalimu iliyotoka mwaka 2020 ikihusu 'mision' chafu ndani ya JWTZ iliyotekelezwa kumuondoa CDF. Kazi hii inapatikana Duka la Kona ya Riwaya, Kinondoni, Dar es Salaam (0655 428 085). Inapatikana pia Kariakoo kwa Helen (0653 254 110) na Morogoro kwa Markus Mpangala (0719 226 293).
Kwa sababu, mwandishi mzuri ni msomaji mzuri, mimi pia napenda kusoma kazi za waandishi wengine. Nimekuwa nikiwafuatilia waandishi wengi sana wa Tanzania na nje ya mipaka ya Tanzania. Navutiwa na nyakati zote za uandishi na waandishi wake tangu utawala wa Shaaban *'Ufukwe'* Robert mpaka utawala huu wa Hussein Issa Tuwa.
Waandishi wote hao wamekuwa na mchango mkubwa sana kwangu.

Kwenye uandishi na hata kwenye kazi yoyote changamoto huwa sehemu ya kulifanikisha jambo hilo. Changamoto kubwa ninayokabiliana nayo ni mtaji na soko la kazi za fasihi.
Soko la kazi za fasihi Tanzania linawafahamu waandishi wachache. Hii ni kwa sababu kuu moja kwamba watanzania wengi hawapendi kusoma vitabu na wanaopenda huwa na waandishi wao. Kitendo cha wasomaji wachache waliopo kuwa na waandishi wao ni tatizo sana hasa kwa waandishi wanaojaribu kujipapatua.
Kwa sababu hiyo, nawahamasisha watanzania tuimarishe utamaduni wa kusoma kazi za Fasihi. Kwenye maandiko ya namna hii kunapatikana maarifa mengi sana. Ikiwa mtu hawezi kumsoma kila mwandishi basi amchague mwandishi hata mmoja na ahakikishe hamalizi mwaka angalau awe amesoma kitabu kipya japo kimoja.

**Penda kusoma vitabu**

JAMVI la SIMULIZI
www.richardmwambe.com

**Faida za kusoma vitabu:**

- Msisimko wa Akili
- Kupunguza Msongo wa Mawazo
- Kuongeza Ujuzi wa mambo mbalimbali
- Kuongeza Msamiati
- Huboresha Uwezo wa Kukumbuka
- Hukupa Uwezo Mkubwa wa kuchambua na kufikiri
- Huboresha Mtazamo na Umakini

Kwetu sisi waandishi, wasomaji ni kundi tunalolitegemea sana. Mwandishi akipata wasomaji ujumbe wake unakuwa rahisi sana kusambaa. Naamini Ipo hazina kubwa kwa kila mwandishi. Hazina hiyo ndio inakusudiwa kuwafikia walengwa (wasomaji).
Waandishi na wasomaji tukishirikiana kwa pamoja (sisi tukiandika na wao wakisoma) tutajenga nguzo kubwa na imara katika kuimarisha utamaduni wa kusoma maandiko.

Ramadhan Makoleko,
Mtwara,
Tanzania.
*+255 (0) 686 778 440*
*rmakoleko@gmail.com*

## NEW IN TOWN: Mimi ni Binti—*Patricia Mwakyeja*


**Anatueleza Patricia Mwakyeja mwandishi wa kitabu 'Mimi ni Binti'**

Kwa sababu mimi ni binti,
Naongea na wazazi naongea na watoto pia. Suala la hedhi bado ni gumu kwa jamii na kuna dhana potofu na mitazamo hasi. Nikaona upo umuhimu kuielimisha jamii na hasa watoto wenyewe kuondoa hofu na kuwa chanya kuweza kusaidiana wao kwa wao pia kuwafanya kuwa salama wanapokua kwenye siku zao. Nimeshuhudia mtoto akianza hedhi au kupata dalili za kuvunja ungo husemwa vibaya na kuhusishwa na tabia za ngono kitu ambacho siyo kweli.

**Anaongezea zaidi...**

Kupitia uzoefu na mazungumzo ya wanawake niliona wazazi wengi wanahofia sana suala la watoto wao kuingia hedhi hivyo hata ujasiri wa kuzungumza nao wanakosa. Siyo kwamba wazazi hawajui wanatakiwa kuongea nini, wanajua kila kitu ila ni waanzishe vipi mazungumzo? Anaona mtoto bado ni mdogo hivyo nikaona nafasi ya kuandika kitabu ili kurahisisha kuanza mazungumzo.

Kukipata kitabu hiki, kwa idadi yoyote ya nakala, wasiliana na mwandishi kwa **0713779494**




## YALIYOJIRI CHANZIGE-TAMASHA LA FASIHI

***Hussein Wamaywa Anashukuru***

HAIKUWA rahisi ila tumefanikisha. Tulifanikisha kufanya vile ambavyo akili zetu zinapenda, mioyo inatamani na roho zinaridhika.

Naam, Tamasha la pili la Fasihi ya Kiswahili 2022 lilikuwa zaidi ya tukio.

Tunamshukuru Mungu na wote waliohudhuria na kutuunga mkono. Hatuna cha kuwalipa, asanteni sana.

***Anasema Kalungwa Matovolwa***

Wasomaji wengi wa vitabu tuna kawaida ya kuchagua vitabu vya kusoma, kila mmoja ana vigezo vyake alivyojiwekea.

Kila msomaji ana vitu vinavyomvutia kutoka katika kitabu, hakuna kitabu cha mwandishi kinachopendwa na kila msomaji, wala hakuna kitabu cha mwandishi kinachochukiwa na kila msomaji.

Msichoke kuandika…

***Mkurugenzi wa Ngurumo ya Mwandishi***

Kwanza tunashukuru sana kwa mwaliko mliotupatia. Tumejisikia furaha kwa heshima mliyotupatia. Japokuwa hatukuweza kufika lakini twaomba mtuwie radhi.
TAFF inaonesha jinsi gani ina kiu ya kuipeleka fasihi mbele na mbali zaidi. Aina hii ya matamasha ni chachu ya kuinua vipaji vichanga vya uandishi. Tuendelee kuwekeza kwa watoto ili kesho tuweze kuiona fasihi ya Kitanzania. Kongole Kwenu!

**Hakikisha unajipatia nakala laini za majarida ya Fasihi nchini. Kila mwezi majarida matatu yanakujia; Ngurumo ya Mwandishi, Tulizo na Kalamu Tulivu.**

**Utayapataje? Wasiliana na wasambazaji wetu kama ifuatavyo, mawasiliano yote kwa WhatsApp**

**NGURUMO : +255 734 514 550, TULIZO: +255 752 353 039, KALAMU TULIVU +255 718 975 659 — Usiwe mchoyo, ukilipata wasambazie na wenzio!**

**PITIO LA VITABU**

# KITABU: VUTA N'KUVUTE

**Katika toleo letu la 14, PITIO LA VITABU tunapitia kwa kifupi kitabu cha VUTA N'KUVUTE kilichoandikwa na Mwandishi Shaffi Adam Shaffi.**

**Kitabu hiki kilichochapishwa mara ya kwanza mwaka 1999 na kuchapishwa tena mwaka 2014 chini ya Mchapishaji Mkuki na Nyota kwa sasa kimetolewa filamu iliyotafsiriwa kama 'Tug Of War'**

Mwandishi anaonesha aina mbalimbali za ukombozi unaohitajika katika jamii. Mfano: ukombozi wa kiutamaduni. Hapa anapinga mila zinazomkandamiza mwanaamke. Kwa mfano, Yasmini kulazimishwa kuolewa na Raza, ni unyanyasaji usiokubalika.

Pia, ukombozi wa kisiasa. Mwandishi anaonesha jinsi ambavyo Zanzibar ilitawaliwa na Mwingereza. Wahusika Denge na Wenzake wanapambana vilivyo kuhakikisha uhuru wa Zanzibar unapatikana.

Ukiachilia mbali aaina hizo mbili za ukombozi mwandishi pia amejadili ukombozi wa kiuchumi na fikra.

## Mapenzi

Mwandishi anajadili mapenzi ya kweli na ya uongo. Katika mapenzi ya kweli, Mwajuma, Denge na kundi lake wana mapenzi ya kweli kwa jinsi walivyopendana wao kama marafiki na jinsi walivyoipenda nchi yao.

## Matabaka

Katika riwaya hii ya Vuta N'kuvute kunajitokeza matabaka matatu

-Wazungu– Hawa waliheshimiwa kuliko matabaka yote. Wazungu wanawakilishwa na wahusika kama Inspekta Wright

-Wahindi - Hawa walifuata baada ya tabaaka la Wazungu. Wahindi wamewakilishwa na wahusika kama Raza, Gulam na wengine wengi.

-Waafrika-Hawa hawakuheshimiwa, walibaaguliwa na kunyanyaswa. Waafrika wamewakilishwa na wahusika kama Denge, Mwajuma, Koplo Matata, Mambo, Sukutua na wengine.

## Mwanamke amewekwa nafasi gani?

Mwanamke katika riwaya hii amewekwa katikanafasi mbalimbali.

-Kiumbe duni asiye na maamuzi yoyote. Yasimini analazimishwa kuolewa na mwanaume asiyempenda kwa sababu tu alionekana duni na asiyeweza kutoa maamuzi.

-Mwenye upendo ws kweli. Mwajuma alimpenda Yasmini hata akakubali waishi wote bila kujali fikra za utabaka na ubaguzi wa rangi uliotawala.

-Mwanamapinduzi asiyependa mila zilizopitwa na wakati. Yasmini anaondoka kwa mumewe, mwanaume ambaye alimuoa pasi na ridhaa yake. Msichana huyu anaamua kutafuta uhuru wake mwenyewe.

-Chombo cha starehe. Yasmini anatumika kumstarehesha Denge na Mwajuma kumstarehesha Mambo

## Kitabu hiki kinatupa ujumbe gani?




www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI

Suala la mapenzi lisiingiliwe na wazazi. Ni vema maamuzi ya yupi wa kuoa/kumuoa waachiwe wale wanaopendana.

Ukombozi wa Sfrika unahitajika kwa gharama yoyote ile. Waafrika waungane ili kupambana na ukoloni mamboleo na aina nyingine za ukoloni ambazo zinaarudisha nyuma maendeleo ya bara hili.

Ukoloni si jambo jema. Mateso wanayoyapata wakina Denge na wananchi wengine yanauchora waziwazi uovu na ubaya wa ukoloni.

Jamii inahitaji Elimu. Ni wakati sasa jamii inahitaji kupata elimu ili iweze kupambana na kuwa huru dhidi ya matatizo mbalimbali.

***Kwa msaada wa Mtandao***

# MAKALA: VITABU KILA MAHALI, KUSOMA SIACHI NG'O!

**Mwezi wa kumi na moja tarehe kumi na tisa na ishirini, katika mji wa Kisarawe tamasha kubwa la kifasihi lilirindima.**

**Vitabu Kila Mahali, Kusoma Siachi Ng'o!**

Hii ilikuwa kauli-mbiu ya tamasha hilo. Ni tamasha la pili kufanyika, linaloandaliwa na Taasisi ya TAFF ya jijini Dar es salaam chini ya Mkurugenzi wake Ndg. Hussein Wamaywa na timu yake.

Siku hizo mbili zilikuwa za moto kwelikweli. Moto wa kifasihi uliwashwa huku mgeni rasmi Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe aliyewakilishwa na Afisa Tarafa akishuhudia nguvu ya fasihi.

Katika tamasha hilo, zawadi kwa washindi wa uandishi wa riwaya miongoni mwa wanafunzi wa shule za Msingi na Sekondari zilitolewa. Shindano hilo la uandishi liliongozwa na mada isemayo

**Faida na Athari za mitandao ya Kijamii hasa Simu za mkononi kwa wanafunzi na namna zinavyochangia kuongeza au kupunguza kiwango cha ufaulu nchini.**




**Picha ya pamoja: Washindi wa tuzo za uandishi wa riwaya kwa shule za Msingi na Sekonari pamoja na Mgeni rasmi na wadau wachache wa TAFF**

## MAKALA: VITABU KILA MAHALI, KUSOMA SIACHI NG'O!

**Washindi wa Mashindano ya Utunzi wa Hadithi Shule za Msingi 2022**

1. Liberata Godfrey Mgavule - Shule ya Msingi Kazimzumbwi
2. Shadya Muhidin Sunga – Shule ya Msingi Masaki
3. Yusra Hamidu Mtonga – Shule ya Msingi Msingi







**Washindi wa Mashindano ya Utunzi wa Hadithi Shule za Sekondari**

1. Wenseslaus Gregory Kidakule - Shule ya Sekondari Kimani
2. Grace Thomas Bavu – Shule ya Sekondari Kimani
3. Boniventure John Chibwana – Shule ya Sekondari Lutheran







Washindi hawa wote walijinyakulia Tuzo, Cheti cha heshima, fulana na pesa taslimu kadiri ya nafasi ya ushindi aliyopata.




**Wengine waliopata tuzo za Heshima ni**

1. Mohamed Hammie Rajab kwa kuitangaza Fasihi ya Tanzania Kimataifa kupitia kitabu cha Maji Mandiga.
2. Profesa M. Mulokozi kwa kuzalisha wadau wengi wa fasihi ya Kiswahili kupitia nafasi yake ya kuwa Muadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
3. Beka Mfaume kwa kuwa Mwanafasihi Mkongwe anayetoa ushauri na malezi kwa wanafasihi wanaoibukia ili watimize malengo yao
4. George Iron Mosenya kwa kuwa mtu wa awali kuonesha njia ya kutumia Tehama kufikisha Fasihi kwa hadhira.
5. Asia Halifa – Kwa kuanzisha kipindi cha kuwasomea hadithi watoto wenye mtindio wa Ubongo na Viungo.
6. Salim Aljabry kwa kuwasapoti waandishi wa Tanzania kwa kununua vitabu vyao bila ubaguzi.

# HADITHI: USIWE MUUAJI—08 Na Jane Davis



**Ilikuwa kazi ngumu mno Kila walipojaribu kupitisha chakula mataya hayakufunguka.Rojo la viazi liliishia kidevuni kabla halijatiririka kushuka kifuani.Wakiwa wanaendelea kuhangaika kumlisha mgonjwa mara wanasikia mlango ukigongwa.**

***Endelea...***
"Atakuwa ni Masunga huyoo"Aliongea mke wa Masanja Kwa sauti ya kunong'ona.

"Shhhh! Usiitike" Mama Masanja aliongea kwa sauti ya chini akimpa ishara mke wa Masanja asiitikie.

Mgongaji aligonga mara tatu mfululizo kisha kukawa kimya, hali hiyo iliwaashiria mgongaji yule tayari ameondoka.

"Hahaha! Tumemuweza kweli leo" Aliongea mama Masanja huku akiendelea kumlisha mgonjwa lakini chakula hakikupita, walipeana zamu zamu hadi wanamaliza rojo lote limeishia kwenye shuka. Walikuwa wamechoka sana walimfutafuta kidogo mgonjwa wao kisha wakamwacha wakitoka mule chumbani.

Walielekea sebuleni ambako hawakumkuta mtu, walipakuwa chakula wakaanza kula. Maneno ya vijembe na mafumbo yalitawala sebuleni hapo muda wote wakiwa wanakula, huku Masunga akiwa chumbani mwake ametulia kimya akiwasikiliza. Hakuwa na neno lolote la kuwajibu zaidi aliwasikitikia sana, aliona kabisa namna wanavyoanza kupotea. Hakutaka kuendelea kuwasikiliza aliwapuuza akawasha redio yake ndogo akawa akasikiliza muziki kwa sauti ya chini hadi akapitiwa na usingizi.

*******
"Hodi jirani nimekupitia,vipi umeshajiandaa?"Alikuwa bi Stumai asubuhi na mapema kasimama wima sebuleni Kwa mama Masanja.

"Karibu jirani, kunipitia kwenda wapi tena?"Aliuliza Mama Masanja.

"Khaa! Mara hii umeshasahau kwani Jana jioni tuliongea nini?"Aliuliza bi Stumai.

"Alaa! Ni kwenda kwa mtaalamu?"Aliongea mama Masanja.

"Asaa! Kumbe!"Alijibu bi Stumai.

"Sasa mbona ni asubuhi sana jirani, kwanini tusiende mida ya jioni hivi"Alitoa wazo mama Masanja.

"Mwenzangu ni mbali Tumbi kule unapafahamu?"Aliongea bi Stumai.

"Khaa! Kumbe mbali namna hiyo, vipi kuhusu usafiri?"Aliuliza Mama Masanja.

"Usijali hilo niachie Mimi tashughulika nalo wewe jiandae chap nakusubiri hapo dukani" Aliongea bi Stumai akatoka kuelekea nje.

Mama Masanja alimimina maji kwenye ndoo ya kuogea akachukua kopo la sabuni akakimbia bafuni kuoga. Alioga harakaharaka akatoka hadi chumbani mwake alijiandaa hadi alipokuwa tayari akabeba mkoba wake hadi nje jikoni.

"Natoka kidogo hakikisha unamwangalia vizuri mumeo" aliongea Mama Masanja akakaza mwendo huyo hadi nyumba ya tatu kulikokuwa na duka la Kijana mmoja wa Kiha waliyezowea kumuita wachu.

"Umechelewa kweli ngoja niite pikipiki tuwahi kuna foleni kweli ya wateja"aliongea bi Stumai akaanza kupiga simu na ndani ya dakika tatu pikipiki mbili za usafiri almaarufu kama bodaboda zilikuwa mbele yao.

Bila kuchelewa walipanda na safari ya kuelekea nje kidogo ya Mji wa Tabora kupitia barabara ya kwenda urambo ikaanza. Kulikuwa na mji mdogo ulioitwa Tumbi ambako pia kulikuwa na chuo Cha kilimo Mati. Mbele kidogo ndipo alipokuwa akiishi mtaalamu wa dawa za kienyeji ambaye bi Stumai alimfahamu.

Pikipiki zile zilikimbia kwelikweli kiasi kwamba abiria wao waliwakumbatia na kuwashikilia vema kwa nyuma. Upepo mkali ulikuwa ukiwapuliza abiria hao kiasi mama Masanja alianza kutokwa na machozi machoni mwake bila kutegemea.

Hakuna marefu yasiyokuwa na ncha hatimaye walifika mji wa Tumbi salama. Pikipiki ziliongo-

za hadi pembeni ya mji kwenye miti miti mingi kisha zikasimama kwenye nyumba moja, nyumba iliyokuwa na kijumba kidogo cha msonge katikati ya uwanja huku pembeni kukiwa na nyumba zingine za tope.

Kulikuwa na foleni ya watu wengi wameketi pale nje, wote walikuwa ni wateja waliokuwa wakisubiri kupatiwa huduma. Bi Stumai na mama Masanja walishuka kwenye pikipiki wakalipa pesa kisha walikwenda hadi walipoketi wanawake wengine wakawasalimia na kuketi pamoja nao hapo.

"Karibuni maziwa na viazi" mwanamke mmoja alifika pale akiwa na ndoo yenye maziwa mtindi na ndoo nyingine ina vikombe. Aliongozana na mwanamke mwingine aliyekuwa amebeba beseni kubwa lililojaa viazi vitamu vilivyochemshwa.

Walianza kuwamiminia maziwa wateja hao mmoja baada ya mwingine. Wakafanya hivyo hivyo kwenye viazi hadi wote wakaenea. Hiyo ndio ilikuwa chai yao asubuhi hiyo, wateja walianza kula taratibu huku wakizungumza stori mbalimbali na matukio ya kijamii.

Muda ulizidi kwenda mteja mmoja mmoja aliingia kilingeni ndani ya kijumba kidogo cha msonge kupatiwa huduma. Hali iliendelea hivyo hadi zamu yao Bi Stumai na Mama Masanja ikafika. Ilikuwa tayari ni mchana na jua liliwaka kwelikweli walikuwa wamechoka kukaa pale, pindi walipoitwa kuingia kilingeni walifurahi mno.

"Twende nyanyuka tuingie" aliongea Bi Stumai akimpiga piga begani mama Masanja aliyekuwa akipiga miayo mfululizo.

"Karibuni karibuni weka sadaka ya wakuu hapa" aliongea mwanamke mmoja aliyekuwa amekaa pembeni ya mtaalamu.

Bi Stumai alifungua pochi akatoka na noti mpya ya shilingi elfu kumi akaiweka pale mbele ya mtaalamu kilipokuwa na vibuyu, shanga, vitambaa vyeusi na mkia wa ng'ombe.
Mwanamke yule pembeni ya mtaalamu aliwasha udi akauweka mbele ya mtaalamu karibu kabisa na uso. Mara mtaalamu yule akiwa kajifunika shuka jeusi akaanza kutikisika.

"Karibuni siiii leteni mikono yenu," aliongea yule mtaalamu kwa sauti nyonyoro ya kike yenye lafudhi ya kiarabu.

Bi Stumai na mama Masanja waliweka mikono yao mbele yule mtaalamu akaishika ghafla akaiachia na kuanza kulia mfululizo.

"Siwezi hapana siwezi hili ngoja aje Mkuu wangu mimi hapana sitaki siiiiii"Aliongea yule mtaalamu kwa sauti ileile ya kike huku akiendelea kulia.
"Wasaidie nakuomba wasaidie,au tukupe chakula kingine"aliongea yule mwanamke pembeni ya mtaalamu.
"Hapana siitaji chochote siwezi kufanya hii kazi ngoja aje Mkuu wangu, naondoka kwaheri siii" aliongea yule mtaalamu akatulia kidogo wakati huohuo yule mwanamke pembeni akamfunua shuka jeusi akamfunika jekundu, ndani ya dakika tu yule mtaalamu akaanza kuunguruma kama Simba.

"Mngruuuum! Leteni mikono yenu" aliongea kwa sauti nzito ya kutisha yule mtaalamu.

Bi Stumai na mama Masanja wakaweka mikono yao mbele ya mtaalamu, akaishika kidogo akaiachia kwa nguvu.

"Mchafuu tokaaa mchafuu wewe mngruuuum nasema toka hufai siwezi kukusaidia mngruuuum" aliongea yule mtaalamu kwa sauti nzito tena iliyojaa ukali, mama Masanja alipoona hivyo alinyanyuka haraka pale chini akimwacha Bi Stumai bado amekaa.

"Tusaidie Mkuu tunakuomba" aliongea bi Stumai.

"Siwezi toka siwezi mngruuuum!"Aliongea yule mtaalamu.

"Mama ondoka mkubwa amekataa" aliongea yule mwanamke pembeni ya mtaalamu akimsihi Bi Stumai atoke nje lakini yeye aling'ang'ania kuendelea kumbembeleza, na Sasa alitoa noti tano za shilingi elfu kumi kumi akaanza kuziweka mbele ya mtaalamu kabla mkono wake haujatua chini. Ghafla yule mtaalamu alimrukia Bi Stumai na kumkaba shingo Kwa nguvu. ……

---

**Riwaya ya Usiwe Muuaji, inaishia hapa katika jarida hili. Nini hatima ya Masanja? Je Bi Stumai atakuwa salama mikononi mwa mganga? Masunga ataamua nini? Usikose kitabu kitakachoibeba riwaya hii na nyingine kutoka kwa mwandishi Jane Davis… Tutawatangazia hapa soon**

# HADITHI FUPI: 40 ZA MUUAJI

## Nelson Ntimba

**Iliku-
wa ni saa kumi na moja ya jioni moja ya mwezi wa tisa, Goodluck alikuwa anafanya mipango ya mauaji yake ya tatu. Alikuwa makini sana kwenye kila hatua aliyoipanga. Alikuwa anafahamu kuua watu kuna hatari sana kama ukilifanya tukio hilo mara kwa mara.**

Mipango hii alikuwa anaifanyia bafuni kwenye nyumba aliyokuwa amekodisha siku chache zilizopita. Kwa dakika kadhaa alitulia kujiangalia kwenye kioo. Uso aliokuwa anatazamana nao kwenye kioo ulikuwa ni mwembamba, ulionesha hakuwa amezeeka sana, lakini alikuwa ameivuka hatua ya kuitwa kijana. Nywele zake zilikuwa ni nyeusi tii, na macho yake yalikuwa ya rangi ya kahawia. Midomo yake ilikuwa ni midogo. Hata yeye mwenyewe hakuwa anavutiwa na midomo yake.

Sauti kutoka jikoni ilimshtua kidogo. Noreen alikuwa anakuja kuoga kabla hajamaliza kupanga mipango yake? Hapana, bado alikuwa na muda wa kutosha. Noreen alikuwa ametoka nje. Alimuona kupitia dirisha la bafuni akienda kwa majirani, na hakulifurahia hilo. Kulikuwa na hatari ya Noreen kutengeneza urafiki na jirani mmoja wapo na hakuwa analitaka hilo litokee kwa sasa.

Hata hivyo, maisha ya ndoa zake tatu  zilizopita yalikuwa yamefuata mlolongo huohuo. Kwa kutumia jina la uongo, angeenda  sehemu ambapo hajulikani na mtu yeyote. Huko alitafuta mwanamke wa umri wa makamo ambaye ana pesa na hana familia. Angemshawishi ndoa, halafu angemshawishi aandike wosia wa kumuachia hela zake. Alikuwa makini sana kuhakikisha anatafuta mwanamke sahihi: Aina ya mwanamke ambaye hatoweza kutengeneza marafiki kwa haraka.

Mary, ambaye alikuwa wa kwanza, alipata ajali mbaya sana akiwa bafuni kwenye nyumba yenye sifa kama hii aliyokuwa amekodisha sasahivi – Ila hilo lilitokea mikoa ya kanda ya ziwa Kaskazini mwa-Tanzania. Polisi walipofanya uchunguzi hawakupata jambo lolote baya. Mtu pekee ambaye alionesha kulikomalia suala lenyewe alikuwa ni mwandishi mmoja wa habari aitwaye Betty. Aliandika  kichwa cha habari ile kwa jina 'KIFO KATIKATI YA FURAHA.' Alikuwa ameweka picha za harusi ya Mary na picha za msiba wake ambao ulitokea wiki tatu baada ya harusi yake.

Doroth, ambaye alikuwa wa pili alimpatia Goodluck changamoto kidogo. Ukweli ni kwamba Dorothy alikuwa na ndugu, tofauti na alivyomwambia Goodluck mwanzoni. Kaka yake Dorothy alikuja siku ya msiba, na aliuliza maswali magumu kuhusu pesa za dada yake. Ilipelekea kufunguliwa kesi mahakamani, lakini Goodluck alishinda.

Yote hayo ilikuwa ni miaka minne iliyopita. Kwa sasa akiwa na jina jipya, na historia mpya ya kutunga, na eneo jipya la kufanyia kazi, Goodluck aliamua kila kitu kipo sawa.

Siku ambayo alimuona Noreen akiwa amekaa peke yake kwenye mgahawa, alifahamu fika huyu ndiye alikuwa mlengwa wake anayefuata. Kilichomfanya ajue ana pesa ni pete ya gharama aliyokuwa amevaa Noreen.

Baadaye aliongea naye. Mwanzoni Noreen hakuonesha ushirikiano, lakini mwisho Goodluck alimshawishi. Baada ya hayo maongezi kila kitu kilienda kama alivyotegemea. Alitumia mbinu za kuonesha mahaba, na wiki ilipoisha Noreen alikuwa amevutiwa naye.

Historia ya Noreen ilikuwa aina ya kitu anachotaka Goodluck. Noreen alikuwa mwalimu kwa miaka kumi, baadaye aliondoka nyumbani kwend kumtibia baba yake mpaka alipofariki. Sasa, akiwa na umri wa miaka arobaini na tatu, alikuwa hana ndugu wala familia, ila alikuwa na pesa ambazo hakuwa anafahamu anazitumia vipi. Na wiki tano baadae toka walipokutana na Noreen walifunga ndoa. Na mchana wa kesho yake waliandika wosia wa kurithishana mali zao zote kwa atakayebaki hai ikiwa mmoja atafariki.

***ITAENDELEA...***

# JULIUS MWITA: NGUVU YA KITABU, SIRI YA UJASIRI WAKE

**Na. Richard Mwambe**

**Ukurasa wetu wa Ana Kwa Ana leo hii, tumesafiri kutoka Iringa mpaka jijini Dar es salaam. Hapa leo, moja kwa moja nakutana na rafiki yangu ambaye kiukweli tumewahi kuonana mara moja tu. Na siku hiyo tulipoonana alikuwa amekuja huko Iringa kwa shughuli za kikazi.**

**Yeye ni mmoja wa wapenzi wa vitabu, naweza kusema kuwa amejenga undugu na vitabu. Na hii ndiyo furaha yetu. Huyu hapa, yeye mwenyewe tumsikilize.**

Naitwa Julius Mwita, nimezaliwa zaidi ya miongo mitatu iliyopita, katika Wilaya ya Serengeti Mkoa wa Mara.
Kielimu nina Shahada ya kwanza ya Usimamizi wa Wanyamapori kutoka SUA.
Kwa sasa ni mjasiriamali na mwanasiasa.

Ninapenda sana kusoma vitabu vya Riwaya za Ujasusi na Upelelezi pamoja na vitabu vyenye visa vya taharuki na kufikirisha.

Usomaji wa vitabu unanisaidia sana katika maisha yangu ya kila siku kwa sababu asilimia 80 ya mambo yanayoandikwa kwenye vitabu ndiyo maisha halisi tunayoyaishi, aina ya watu na tabia zao, namna ya kuishi nao kulingana na mazingira niliyopo.

Vyote vinakuwa kwenye vitabu na maarifa niyapatayo kwenye vitabu husika huwa yananisaidia kukabiliana na kutatua Changamoto nyingi sana za kimaisha.

Vitabu vikisomwa kwa tafakuri jadidifu, husaidia sana katika kubadili maisha ya mtu hasa kumweka



kwenye mwelekeo chanya. Mathalani vitabu vingi vya kijasusi na Upelelezi huhusiana na masuala muhimu kama biashara ya dawa za kulevya, ufisadi ndani ya Serikali, biashara ya meno ya tembo, biashara ya usafirishaji haramu wa binadamu ambavyo mara nyingi hueleza athari za mambo hayo ambayo husaidia kumuelimisha mtu ili aweze kuelewa na kuyaishi mazingira anuai na mahalia.

Mimi ni mjasiriamali na Mwanasiasa.

Kuna tatizo kubwa la jamii ya Watanzania kutokuwa na utamaduni wa kusoma vitabu.

Hii inasababisha hata fani ya uandishi wa vitabu kuonekana haina maslahi, ilhali katika nchi kama Kenya, Zambia, Afrika ya Kusini, Misri, Morocco nk usomaji wa vitabu ni utamaduni unaojengwa kuanzia katika ngazi ya familia.

Ukienda nchi nilizozitaja hapo na nchi za Ulaya katika kila nyumba huwezi kukosa aghalabu shelfu ya vitabu kadhaa ambavyo husomwa na wanafamilia husika.

Hivyo, nawasihi Watanzania wajitahidi kujijengea utamaduni wa kusoma vitabu kulingana na mambo wanayoyapenda, mathalani mtu anayependa hadithi za mapenzi anaweza kusoma vitabu vya riwaya za mapenzi na kujielimiaha zaidi eneo hilo.

**Asante sana Kamanda Julius Mwita. Kama alivyosema hapo awali yeye mwenyewe kuwa ni mjasiriamali na mwanasiasa. Ni kijana jasiri, mpambania haki, asiyeogopa. Leo nimejua kumbe vitabu hasa riwaya za kijasusi na kipelelezi ndivyo vinamjengea ujasiri katika uga wake wa maisha.**

**Asante sana na salimia**

# MPIGA MBIO — 14

**"Anaijua Mungu tu!" Jibu la Ikunda liliwafikia wale askari waliokuwa na Habibu garini, wakacheka. Habibu alijiinamia kwa sekunde kadhaa bila kuongea lolote. Kwa namna moja au nyingine alijisikia aibu.**

**Endelea...**

Donge la hasira lilimkaba shingoni, akajiapia moyoni kuwa lazima amfanyie jambo mwanamke huyo. Walimpita na lile gari na kuondoka zao. Ikunda aliitoa simu yake kwenye pochi na kuanza kumpigia huyo anayemtaka. Hatua kama kumi hivi alisimama kusubiri simu ile ipokelewe. Kimya! Inaita na kukatika. Ikunda akahisi moyo kumuingia ganzi. alikuwa akimpigia Kenneth, waridi la moyo wake.

*** *** ***

Taarifa za wizi uliotokea zilisambaa kasi sana. Yule Muindi alikwenda kuripoti kituo cha polisi cha Salenda akiwa kachanganyikiwa, hana hali. Milioni kumi na saba zilikuwa zimeondoka kimzaamzaa tu.

"Unaweza kuikumbuka sura ya huyo mtu?" askari aliyepokea suala lile alimuuliza mlalamikaji.

"Mimi siwezi kukumbuka, labda dereva wangu…" akajibu. Yule polisi akamgeukia yule kijana.

"Enhe…" akamtaka kusema. Yule kijana akaeleza tukio zima lilivyotokea. Kwa maelezo yake, wale polisi wakatazamana. Mmoja akamwambia mwenzake, "Walewale!"

"Ndiyo mtindo huuhuu waliutumia kumwibia yule Mkongo… lakini kwa nini watu hawataki kuelewa kila tunapowaambia kufunga vioo na milango wakiwa na pesa nyingi garini!" akalalama. Wakaendelea kuwahoji na kuchukua maelezo. Kisha wakawaruhusu waende na kuwaahidi kulishughulikia haraka iwezekanavyo.

"Sasa Kanjibhai, sisi tutafuatilia halafu tutakupigia simu… lakini kuna hitajika hela ya mafuta ya gari la kuzungukia…" askari mmoja alimwambia. Mlalamikaji kaja kulalamika kaibiwa pesa halafu na wao wanaomba pesa ya mafuta, kwani yale ya serikali yanafanya nini? Rushwa! Tatizo sugu kwenye vituo vya polisi. Yule Muindi akajipigapiga na kutoa shilingi elfu thelathini, akawakabidhi.

"Hawa jamaa wanatuchezea akili…" askari mmoja akamwambia mwenzake.

"Jana ilikuwaje? Si vijana walienda Stereo kuwakamata! Maana yule Mkongo naye kaweka dau zito…" mwingine akamjibu.

"Wamemkosa! Tatizo aliyetupa taarifa naye hakuwa anaeleweka; mara yuko mmoja, mara wawili, sasa lipi ni lipi?" yule askari akasema huku akiweka vizuri yale maelezo tayari kwa kufungua jalada.

*** *** ***

Simu ya Kenneth iliita kwa fujo. Alipotizama, aliona ni Ikunda, hakupokea. Alisita. Tayari alikuwa katika nyumba yake huko Ununio. Ule mkoba ulishachomwa moto na pesa kusundwa mahali salama.



Richard Mwambe

Kebby na Scogon nao kila mmoja alikuwa mahala pake. Kila mtu alikuwa akifuatilia matangazo ya redio ili kujua nini kipo huko duniani.

Mlio wa simu uliofuata ndiyo uliomwinua kitandani. *RPC!*

"Kijana nimesikia kazi yenu, najua leo mmenona… tuonane palepale pa siku zote muda uleule, mje au uje na kitu kinachoeleweka…" yule RPC akampa maagizo Kenneth.

"Sawa afande!"

**Saa kadhaa baadae...**

Kenneth aliwasili eneo la Makaburi ya Kinondoni jioni ya saa kumi na moja. Alililivuka geti na kuvuta hatua kama anaelekea Hananasif. Baada ya kupita makaburi kama ishirini hivi, akawasili pale anapopataka. Ukimya uliotawala eneo hilo uliogofya kwa namna moja au nyingine. Akasimama Mbele ya kaburi moja kubwa lililojengwa kisasa. Kama ungemwona alivyovaa nadhifu, ungejua hakika ni ndugu wa marehemu. Maana viwalo vyake gharamaze zinashahabiana kabisa na muonekano wa kaburi lile.

# MPIGA MBIO — 14



www.richardmwambe.com JAMVI la SIMULIZI

Dakika tatu baadae, gari moja likaingia katika wigo wa makaburi hayo. Toyota Hilux Double Cabin jekundu, lililowekwa vyoo vya giza. Likasogea taratibu mpaka pale alipo Kenneth, jirani kabisa na kusimama.

Kenneth alivuta hatua kuliekea lile kaburi, akaweka ua juu yake na kufanya ishara ya msalaba. Akageuka na kuliekea lile gari. Akafungua mlango wa mbele kushoto na kuketi.

Nyuma ya usukani alikuwapo RPC mwenyewe, Mzee Kitwana. Mzee Kitwana kama alivyojulikana mtaani anapoishi alikuwa mkuu wa polisi jijini Dar es salaam. Alihamishiwa hapo kutokea Mwanza alipofanikiwa kupambana kwa weledi na nguvu zote dhidi ya uvuvi haramu na kuukomesha kabisa. Sifa zake zilifanya ahamishiwe hapo Dar es salaam ili akomeshe mtandao wa ujambazi uliokithiri na kuhatarisha usalama wa matajiri.

Katika kazi yake hiyo, ndipo alipofahamiana na vijana hawa, yaani Kenneth, Kebby na Scogon. *Smart guys,* aliwaita hivyo.

Hakuongea neno, alinyosha kiganja chake tu. Kenneth aliingiza mkono ndani ya koti na kuchomoka na bahasha ya kaki iliyofungwa vizuri.

“Ngapi?” Mzee Kitwana akauliza.

“Tatu!”

“*Ok! Very good*” alijibu huku akipokea. Akafungua droo ya gari lake na kuzisweka humo. “Ila muwe waangalifu, mkiona sehemu inakuwa hatarishi basi msitishe operesheni, sawa?”

“Sawa!” Kenneth akajibu. Lile gari likaondoka kuekea Hananasif na kumwacha kijana huyo huko.

*** *** ***

Mwananyamala Inn ilipomkea Kenneth majira ya saa mbili usiku. Meza aliyoketi alikuwa peke yake. Dakika chache baadae alikuwa na bia mbili mbele yake, zote zilifunguliwa. Alikunywa taratibu huku akiangalia saa yake kila baada ya muda mfupi.

Alionekana kama mtu mwenye miadi na mwenzake. Hakutulia. Ni kweli, haikupita nusu saa mwanamke mrefu, mwembamba, mweupe mwenye pua ya Kiarabu aliungana naye. Wakaketi kwa mtindo wa kutazamana. Hata alipokuja mhudumu, hakuagiza chochote.

“Mchongo si mmefanikiwa?” yule mwanamke akamuuliza Kenneth.

“Kwa asilimia zote!” akamjibu, kisha akachukua kinywaji chake na kupiga mafunda kadhaa. “Nilikuwa nina wasiwasi sana, lakini Siku ileile ilimachua!”

“Huwa sina kazi mbovu Kenny… ile teknolojia ya Uswizz siyo Nigeria. Si unajua vile vitabu vinatoka Swizz… hukohuko, sasa…” yule mwanamke akasema kwa majigambo. Kenny akamjibu kwa kutikisa kichwa.

“Haya nipe changu nisepe…”

Kijana akaingia ndani ya koti na kutoka na bahasha iliyononа, akampatia.

“Tano!” akamwambia.

“Asante…” akamshukuru na kuinuka tayari kwa kuondoka. Dakika chache baadae akabaki tena peke yake. Na hapohapo simu yake ikaita kwa Fujo. Alipoitazama, Ikunda. Akainyayua na kuiweka sikioni.

“Jamani Kenny wangu, leo hupokei simu… unaniweka njia panda, unanitesa!” sauti ya Ikunda ikalalamika simuni.

“Siyo hivyo mpenzi! Nilikuwa bize na kazi na simu niliitupa mbali! Baadae nikaona *call* zako halafu nikasahau kukupigia…” Kenny akamjibu.

“Loh! *Sweetie*… mekumiss mie… njoo basi…” Ikunda akachombeza kwa urai wa mapenzi. Mwili wa Kenny ukasisimka. Afanyeje? Hakuwa na jambo jingine la kufanya jioni hiyo. Isiwe tabu! Kenny alijinyanyua tayari kwa safari ya kwenda kwa Ikunda. Akauendea mlango mkubwa wa kuingilia kwenye baa hiyo. Alipoufikia tu, akasita. Akasimama na kutazama vizuri kama kile anachokiona ni sahihi au la! Akatazama nyuma, watu waliendelea na starehe zao. Akatazama mbele alichokiona bado kilikuwa kikiendelea. Hakuelewa kama macho yake yako sahihi au lah!

***Itaendelea...***

# SHUBAKA LA VITABU

**SHUBAKA LA VITABU**: Katika toleo hili la kumi na nne tumekuja na safu mpya ya Shubaka la Vitabu. Najua utajiuliza shubaka la vitabu ni kitu gani. Ndiyo, hata mimi mara ya kwanza ilinibidi niombe ufafanuzi kuelekwa maana yake kwa usahihi. Na wajuvi wa hilo walisaidia kunieleweshа

Katika safu hii ambayo tutakuwa nayo hapa leo, tutazungumza machache na mwanadada **Vennita Mwita.** Yeye kama mpenzi wa usomaji wa vitabu ana shubaka lake pale nyumbani na ndilo hasa tunalolizungumzia. Hii itakuwa ni *Challenge* kwa wasomaji wa vitabu. Hivyo wahi mapema kwa toleo lijalo ili nawe utambe na shubaka lako

Naitwa Vennita Mwita,
Mimi napenda kusoma vitabu vya aina mbalimbali (mada). Mfano hadithi, motivation, na vya kuongeza maarifa.

Mara nyingi nasoma nikiwa nyumbani au wakati mwingine napenda kwenda kwenye fukwe ili kusoma, pia niwapo safarini hutumia muda mwingi kusoma. Kitabu kikiwa kitamu sana basi hata kitandani nakuwa nacho tuu hadi usingizi utakapo nipitia.
Lakini pia naweza kusoma tena kitabu nilichowahi kusoma zamani …

***Kuhusu shubaka lako… tujuze***
Shubaka langu lina vitabu mbalimbali, mfano encyclopedia, kamusi, maswala ya masoko, hadithi, hadithi za watoto, mapenzi, mapishi, uongozi, Elimu, sheria, katiba ya URT etc
*(URT—United Republic of Tanzania)*

Shubaka langu nilitengeneza jinsi nipendavyo mie. Juu naweka vitabu na chini naweza kukaa na kusoma au kuandika .

***Maana yake lina rafu kwa juu humo ndani na meza upande wa chini.. Waoh! Wonderfull***
Nilitengeneza hususani kwa ajili ya vitabu, linakaa katika chumba maalumu cha kusomea, haliko sebuleni

***Unaringaaaaa mwenyewe, eti?***
Ndiyo, kila nitazamapo shubaka langu, nafurahia kuona uwezo wangu wa usomaji unakua lakini pia naona jinsi ambavyo sijasoma vitabu vingi zaidi, hivyo napaswa kuongeza bidii ya kununua na kusoma.
Ila kwa sasa naona ni dogo, napaswa kuweka katika mpango hivi karibuni, kuwa na shubaka jipya na kiti kizuri zaidi cha kusomea


***Zaidi ya hapo… shubaka lako lina umuhimu gani?***
Lina umuhimu sana, huwa lanikumbusha kuwa napaswa kuprint kitabu (vi) changu pia ili niongeze katika idadi na kuwafikia wasomaji wangu vyema zaidi.

***Vennita Mwita...***
***Asantee.***



# KITABU NILICHOSOMA

**Mwl. Juliana Isondo**




Mwandishi anasema nidhamu binafsi (*self discipline)* inahitajika katika kila idara ya maisha yetu ya kila siku.
Sambamba na hili nimejifunza yafuatayo

1. Hasara za kukosa nidhamu, mojawapo anasema mtu anapokosa nidhamu ni ngumu sana kutimiza malengo yake.

2. Watu wengi hawapendi mabadiliko kwasababu ya uoga wa kuchekwa hasa pale watakaposhindwa kutimiza malengo.


3. Watu wote waliofanikiwa katika maisha walifeli kwanza. Kufeli ni sehemu ya maisha.

4. Nidhamu na mpangilio ni vitu viwili visivyotenganishwa. Anamaana kuwa ili uweze kufanikisha malengo yako ni lazma uwe na mpangilio mzuri wa mambo na vitu vyako.

5. Watu wengi hawapo tayari kulipa gharama za mabadiliko. Unapoamua kubadili tabia fulani ambayo hupen-



dezwi nayo usiogope maneno ya watu, marafiki na hata ndugu.




Kitabu ni kizuri saaana.
Hapo sijakimaliza ila kinavutia kukisoma.

---

Kutana na Mwanamke aliyepitia magumu katika usichana wake. Alibeba mimba akiwa binti mdogo. Kabla ya miaka 25 alikuwa tayari na watoto watatu.
Yeye ndiye kichwa cha familia, anayetegemewa na watoto wake.

Akaamua kuacha kazi ya kuajiriwa akiwa mjamzito na kufanya jambo alilolipenda na lililobadilisha mustakabali mzima wa maisha yake.
Pamoja na maisha yenye milima na mabonde amefanikiwa kutengeneza pesa ndefu. *(Yeye anaita six figures per year!)*
Nimejifunza vingi vichache vyake;

1. Kujenga mahusiano ni muhimu zaidi kuliko kuuza bidhaa.

2. Kitu cha kwanza katika biashara ni upendo na huduma. Ukiuza kwa upendo utauza zaidi.

3. Ukifanikiwa kutengeneza pesa nyingi usipandishe gharama za maisha yako. Live below your means.

4. Nyuma ya mafanikio ya watu kuna vipindi vigumu ambavyo mfanyabiashara hupitia na maranyingi huwa havisemwi.

5. Mwenye kiu ya mafanikio anapaswa kuwa mwanafunzi wa kudumu.

**Tujifunze, hii ndiyo maana nzima ya Kitabu Maisha**

**Tangazo**




Kwa maziwa bora kabisa ya mtindi usioghoshiwa, wasiliana nasi ABBYMILK tukuhudumie. Kunywa maziwa kwa afya yako.

Tunatoa huduma kwa wauzaji wote, wa jumla na rejarejaa. Unaujua mtindi OG wewe? Jaribu leo ABBYMILK

Kwa mawasiliano tupigie **+255 627 129 136**

---

www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI

Jarida hili hutolewa na Jamvi la Simulizi kila mwezi
jamvilasimulizi@gmail.com